# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

***Dar es Salaam***
***23 Juni, 2025***

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anatarajia kuondoka nchini kesho tarehe 24 Juni, 2025 kuelekea Maputo, Jamhuri ya Msumbiji ambapo atakuwa na ziara ya kikazi ya siku mbili.

Rais Dkt. Samia anatarajia kuwa Mgeni Rasmi katika Sherehe za Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Jamhuri ya Msumbiji, kufuatia mwaliko maalum wa Rais wa nchi hiyo, Mhe. Daniel Francisco Chapo, ambazo zitafanyika katika Uwanja wa Machava, Mjini Maputo.

Itakumbukwa kwamba, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa wapigania uhuru wa Msumbiji na ilitoa mchango wa hali na mali kuunga mkono harakati za ukombozi wa Taifa hilo.

Akiwa nchini humo, Rais Dkt. Samia atatembelea eneo la Kumbukumbu ya Mashujaa wa nchi ya Msumbiji *(Mozambican Heroes' Square)* ambapo atatoa heshima zake na kuweka shada la maua kama ishara ya kuwaenzi waliopoteza maisha wakati wa harakati za mapambano ya uhuru wa nchi hiyo.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu